OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

HOTUBA YA MHE. HAMZA S. JOHARI – MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI KATIKA MKUTANO WA WATUMISHI WA OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI, TAREHE 28 APRILI, 2026

Mhe. Dkt. Juma Zuberi Homera, Waziri wa Katiba na Sheria;

Samwel M. Maneno, Naibu Mwanasheri Mkuu wa Serikali;

Menejimenti yote ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;

Watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;

Wageni Waalikwa;

Wanahabari;

Mabibi na Mabwana.

Kazi na Utu …….. !

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali …… !

Mhe. Mgeni Rasmi na Watumishi wenzangu wa OMMS;
Awali ya yote na kwa unyenyekevu mkubwa, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Rahim mwingi wa Rehema kwa kuturuzuku uhai na afya njema na kutuwezesha kukutana leo kwenye Mkutano wa watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Tangu tukutane mara ya mwisho, wapo wenzetu waliotwaliwa kutoka katika ulimwengu huu. Pamoja na wengine wote, tumkumbuke na kumuombea aliyekuwa mtumishi mwenzetu na Mkurugenzi Msaidizi Divisheni ya Mikataba Bi. Mukabatunzi D. Rwakilomba ambaye alifariki tarehe 28 Oktoba, 2026.

Tuendelee kuwaombea ndugu, jamaa, marafiki na familia zao ustahimilivu na amani. Daima tukumbuke kuwa, *Sisi sote ni wa Mwenyezi Mungu, na kwake sote tutarejea.*

Shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa imani yake kwangu na kuniteua kwa awamu nyingine tena kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ahadi yangu kwake ni kuchapa kazi kwa bidii ili kumsaidia yeye na kuwatumikia wananchi wetu.

Imani ya Mheshimiwa Rais kwangu inatokana na namna ninyi watumishi wenzangu wa Ofisi hii, mlivyonisaidia kwa weledi, uadilifu, uhodari na kwa bidii yenu katika kuyatekeleza majukumu yetu ya kuishauri Serikali katika masuala ya kisheria.

Nimshukuru Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Menejementi na ninyi watumishi wenzangu wote kwa kuendelea kunipa ushirikiano unaoniwezesha kuyatekeleza kwa ufanisi majukumu yangu ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Mgeni Rasmi na Watumishi wenzangu wa OMMS;
Nikupongeze Mheshimiwa Dkt. Juma Zuberi Homera, Waziri wetu wa Katiba na Sheria kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Waziri wa Katiba na Sheria. Pia kipekee, nichukue nafasi hii, kukushukuru kwa dhati ya moyo wangu, kwa kukubali mwaliko wetu wa kuja kufungua kikao hiki muhimu cha watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kwa niaba ya Ofisi yangu, tunasema asante sana.

Mhe. Mgeni Rasmi na Watumishi wenzangu wa OMMS;
Tangu kuteuliwa na kuapishwa kwangu tarehe 5 Novemba, 2026, hili linakuwa kusanyiko langu kubwa la kwanza kuhusisha watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Hivyo nina furaha sana kwa siku hii, na ombi langu kwenu, tukakitumie kikao hiki kulifikia lengo la sisi kukutana hapa. Twendeni tukazungumze pamoja leo, tukatoe michango yetu na maoni yetu kwa uhuru na uwazi.

Nikupongeze sana Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Sekretarieti yote, kwa maandalizi na hatimaye kufanikisha shughuli hii kubwa na muhimu kwa ustawi wa Ofisi yetu na Taifa kwa ujumla.

Na kwa sababu ya umuhimu wa kikao hiki, nitaomba niseme machache ingawa kwa urefu kidogo.

Mhe. Mgeni Rasmi na Watumishi wenzangu wa OMMS;
Kwa kufanya vikao kama hivi, ndipo tunapotekeleza kwa vitendo dhana ya uongozi shirikishi ambao moja ya nguzo zake muhimu ni uwepo wa mifumo madhubuti ya mawasiliano na majadiliano iliyopo kati ya Menejimenti na Watumishi wote.

Katika kitabu cha Mhubiri, Sura ya 4 na Mstari wa 9 imeandikwa:

> *"Afadhali kuwa wawili kuliko mmoja, kwa maana faida yao kwa kazi yao ni nzuri. Kwa maana wakianguka, mmoja atamwinua mwenzake."*

Ndugu zangu, tuko hapa leo hii kwa sababu sote tunahitajiana. Hakuna Mkurugenzi wala Wakili wa Serikali, hakuna Wakili wa Serikali wala Mwanahabari au Msaidizi. Hakuna Idara Ndogo au Saidizi, bali katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuna timu moja kubwa.

Ndugu Watumishi wenzangu wa OMMS;
Leo hii, pamoja na kuwa tumekutana kuzungumza, kujadiliana na kubadilishana maarifa, ujuzi na uzoefu tukiwa kama familia moja, lakini pia tutakuwa na majukumu mengine kadhaa ikiwemo:

i. Uzinduzi wa Website Mpya ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;
ii. Kuwapitisha Watumishi kwenye Muundo mpya wa Ofisi ulioidhinishwa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 04 Machi, 2026,
iii. Kuzindua mfumo wa NesT na OAG-MIS kuhusu Upekuzi wa Mikataba,
iv. Kujadili kuhusu Mwongozo wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa Mawakili wa Serikali kuhusu kufanya kazi za uwakili; na
v. Kuwapitisha watumishi kwenye Taarifa ya Utendaji ya mwaka 2025/2026 pamoja na Mpango na Bajeti ya mwaka 2026/2027.

Ndugu Watumishi wenzangu wa OMMS;
Yapo mambo kadhaa ambayo kwayo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali tunajivunia na kwa hakika tunapaswa kuyasema kwani ni mafanikio ya bayana. Leo hii akitokea mtu mmoja anayetufahamu vizuri, akatutazama au kutuuliza kwa habari ya tulivyo sasa na tulikotoka, ni wazi kuwa atastaajabu!

Ili kufahamu hatua tulizopiga au tumefanikiwa kwa kiwango na namna gani, ni lazima tufahamu tumetoka wapi. Mwanazuoni mmoja maarufu mwenye asili ya Kenya aitwaye Prof. Ali Mazrui aliwahi kunukuliwa akisema:

> *"Mtu asiyejua alikotoka hajui anakokwenda"*

Kwenye vikao vyangu vyote na mabaraza baina yangu na ninyi, ndani ya mwaka mmoja tu uliopita, vilio vyenu wakati wote vilikuwa ni uduni wa maslahi, upungufu wa motisha kazini, ukosefu au uhaba wa vitendea kazi muhimu kama magari, kompyuta mpakato na vinginevyo, upungufu wa watumishi, ukosefu wa mafunzo kazini, ushiriki wa shughuli za michezo, na kadhalika. Changamoto hizi, zilitufanya sisi viongozi wenu tusilale, tukapambana usiku na mchana ili kuhakikisha changamoto hizi zinabaki kuwa simulizi.

Mhe. Mgeni Rasmi na Watumishi wenzangu wa OMMS;
Kwa ufupi mniruhusu tufahamishane kama si kukumbushana yale ambayo yamefanywa na Serikali yetu chini ya uongozi wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Ofisi yetu:

i. Mazingira ya kazi ya watumishi yameboreshwa kwa kiasi kikubwa sana. Kwa mfano;
    - Uwepo wa chai ya asubuhi na chakula cha mchana bila malipo kwa watumishi wote wawapo kazini; na
    - Uwepo wa usafiri wa kuwachukua na kuwarudisha watumishi majumbani.

ii. Ofisi imeajiri jumla ya watumishi wapya Kumi na Tano (15) na kupokea jumla ya watumishi Ishirini na Nne (24) kwa njia ya uhamisho;

iii. Jumla ya watumishi Sabini na Tano (75) wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi nje ya Nchi, watumishi Mia Moja na Nane (108) wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi ndani ya Nchi na watumishi Kumi na Sita (16) wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu ndani na nje ya nchi katika nyanja mbalimbali;

iv. Mawakili wa Serikali wamejengewa uwezo kwa kupatiwa mafunzo ya kisekta kupitia Taasisi mbalimabli kama vile; TASAC, NEMC, TPDC, MC, PSSSF, PPPC, TIRA, PURA na TANESCO;

v. Tumefanikisha kuwa na kifurushi maalum cha nyongeza cha huduma ya Bima ya Afya (NHIF) kwa watumishi wote (Supplimentary package);

vi. Maslahi ya watumishi wetu wote yameboreshwa kwa kiwango kikubwa sana (kwa utani wanaita dubwashika). Kwa mfano;
    - Posho za mavazi kwa watumishi wote.
    - Posho za simu kwa watumishi wote.

- Posho ya pango kwa watumishi wote.

vii. Kununuliwa vitendea kazi vipya, ikiwemo kompyuta mpakato, CCTV camera, samani za Ofisi na vingine vingi kwa watumishi wote na kwa matumizi ya Ofisi;

viii. Jumla ya magari mapya tisa (9) yamenunuliwa na kati yake sita (6) tayari yamepokelewa na yanatumika;

ix. Ofisi zetu za mikoa zimewezeshwa na kuimarishwa kibajeti, vitendea kazi na rasilimali watu. Mathalani; Mikoa ya Mbeya, Mtwara, Kagera, Mwanza na Tanga imepatiwa magari na Mikoa yote imeongezewa Mawakili wa Serikali;

x. Tumekamilisha utaratibu wa kuanzisha Ofisi tisa za mikoa ya; Morogoro, Kigoma, Katavi, Songwe, Ruvuma, Singida, Shinyanga, Mara na Tanga; na mara tu taratibu za kiutumishi zitakapokamilika, Ofisi hizo zitafunguliwa kabla ya tarehe 31 Juni, 2026;

xi. Ushiriki wa watumishi katika michezo umeimarishwa na Ofisi imewawezesha washiriki wote wa michezo kwa namna mbalimbali.

Ndugu Watumishi wenzangu wa OMMS;
Uko usemi unaosema;

“Mfanyakazi anayethaminiwa hutoa kazi yenye thamani”

Leo hii, sote ni mashahidi wa namna Ofisi yetu kwa uwezeshwaji wa Serikali ya awamu ya sita tulivyopiga hatua katika kutatua changamoto za watumishi na za Ofisi kwa ujumla. Yaliyofanyika ni mengi, na kwa muda tulionao hayatoshi kuelezwa, nanyi watumishi wenzangu ni mashahidi wa haya yote.

Kwa kuzingatia muda uliotumika kuwezesha mafanikio hayo, mtu mwingine angefikiri ni hadithi na kamwe asingeamini kama yangeweza kufanyika.

Kwa haya makubwa yaliyowezekana katika kipindi hiki kifupi, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitarudia tena kumshukuru, kwa dhati kabisa ya moyo wangu, Rais wa Nchi yetu, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo Serikali yake imewezesha hayo kufanyika. Asante sana Mhe. Rais.

Ndugu Watumishi wenzangu wa OMMS;
Pamoja na utatuzi wa changamoto na mafanikio makubwa yaliyopatikana, tunakiri na kutambua kuwa zipo changamoto ambazo bado zinaendelea kutatuliwa; wakati mwingine unapofanikisha mambo fulani, au unapotatua changamoto fulani, huibuka changamoto mpya. Niwaahidi leo, sisi viongozi wenu kwa kushirikiana nanyi nyote, tutaendelea kuhakikisha kuwa, tunazitafutia ufumbuzi changamoto kwa haraka kadri zinavyojitokeza.

Mhe. Mgeni Rasmi na Watumishi wenzangu wa OMMS;
Kwako Mhe. Waziri na Mgeni Rasmi wetu leo;

Kwa niaba ya Menejimenti na umma huu wa watumishi wa Ofisi yangu, tunaahidi wakati wote tutashirikiana kikamilifu pamoja nawe na Wizara yetu kwa ujumla katika utekelezaji wa majukumu yetu na zaidi katika azma yetu kuu ya kuwahudumia Watanzania, huku daima tukiongozwa na kauli mbiu yetu: “Weledi na Ubora”.

Tutatendelea kutekeleza majukumu yetu kwa kuzingatia Katiba, Sheria, Kanuni, Taratibu, Dira na misingi ya Taifa letu. Wakati wote tutakumbushana juu ya umuhimu wa uzalendo kwa kuilinda tunu ya amani ya nchi yetu.

Kwa watumishi wenzangu;
Ningependa kuwashirikisha mambo yafuatayo muhimu:

i. Kwa kutambua kuwa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi kwa wafanyakazi ni uwekezaji wa uhakika, tutaendelea kuhakikisha watumishi wote wanapata mafunzo husika kwa kadri ya mahitaji ya watumishi na Ofisi yetu;

ii. Tutaendelea kuwa na vikao na mikutano ya pamoja kama hii, tukiamini kuwa, sauti moja inaweza kunong’ona, lakini sauti zetu zote kwa pamoja ni ngurumo ya maendeleo ya Ofisi na Taifa;

iii. Ujenzi wa Ofisi yetu ya Makao Makuu Mtumba, Dodoma na Ofisi za Mikoa ya Arusha na Mwanza unaendelea;

iv. Vitendea kazi vya Ofisi ikiwemo magari na samani vitaendelea kununuliwa kulingana na upatikanaji wa fedha na mahitaji ya Ofisi;

v. Tutajitahidi kila mara, kuendelea kuboresha mazingira ya kazi na ya watumishi kila mara nafasi itakaporuhusu;

vi. Mwisho, leo sote tuna furaha kutokana na maboresho yaliyofanyika. Ni matumaini yangu kuwa, tukikutana wakati mwingine, tutasimulia hadithi nyingine nzuri kuhusu maboresho ya mishahara yetu. Mwenyezi Mungu atulinde.

Ndugu Watumishi wenzangu wa OMMS,
Tumeshuhudia changamoto zenu nyingi kama si zote zikitatuliwa na tumejionea mambo makubwa yakifanyika; deni linalobaki ni kwetu na kwa pamoja tunayo kazi ya kulilipa. Ni matarajio ya Serikali na wananchi kuwa, kila mmoja katika eneo lake atakwenda kuwajibika na kutekeleza majukumu yake kwa kujitoa, uaminifu, umakini, weledi na ubora unaotarajiwa.

Surah At-Tawbah 9:105 inasema;

“Fanyeni kazi, kwani Mwenyezi Mungu atauona utendaji wenu, na Mtume wake na Waumini …”

Mnamo tarehe 17 Julai, 2025 wakati wa uzinduzi wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya miaka 25, maarufu kama “Dira 2050”, Mhe. Rais aliueleza Umma wa watanzania kuwa, ili kufikia dira ya kuwa Nchi ya Uchumi wa Kati Ngazi ya Juu unaoongozwa na maarifa na uchumi wa viwanda, ni lazima kila mmoja wetu ajenge na kudumisha utamaduni wa uwajibikaji unaozingatia weledi, ubunifu katika utekelezaji wa majukumu mbalimbali.

Katika hilo, nikiwa kama Mkuu wa Ofisi, ningependa nitoe maelekezo yafuatayo;

Twendeni tukawajibike kweli kweli. Wananchi wetu wanataka kuona kutoka kwetu matokeo bora ya kazi zetu. Nirudie tena, twendeni tukachape kazi.

> *“Kazi yako ndiyo sala yako. Ifanye kwa moyo wa bidii na kwa ubora.”*
> Wakolosai Sura ya 3 na Mstari wa 23.

Mkurugenzi wa Huduma za Ushauri na Uratibu (DCAS);
Tunafanya kazi nzuri. Ningependa pamoja na timu yako mkajipange zaidi. Muongeze ubunifu katika kazi zenu, mkabuni zaidi mkihakikisha kuwa, wakati wote, ubora wa ushauri wetu unaakisi hadhi na heshima ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kazi zetu zote zitokane na utafiti wa kina, na wakati wote zipitiwe na kuhakikiwa kwa umakini unaotakiwa.

Mkurugenzi wa Mikataba;
Tukirejea kazini, tukaongeze kasi, tukakimbie sio kwa pupa wala msukumo wowote, bali kwa weledi na ubora zaidi. Ushauri wetu wa kitaalamu katika upekuzi, utambulike na uheshimike kwa ubora wake. Mkatafiti kwa kina na kuhakikisha kazi zote zinapitiwa ipasavyo.

Mkurugenzi wa Rasilimali Watu na Mali;
Kahakikishe watumishi hawa, wanaenenda na kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma na wakati wote wanazingatia maadili ya msingi ambayo ni:

- Weledi
- Ubunifu
- Uadilifu
- Uwazi
- Uwajibikaji na
- Ushirikiano

Hakikisha rasilimali zote za Ofisi yetu, kuanzia majengo, magari, vifaa vya kielektroniki, samani na kadhalika, vinatumiwa na kulindwa kwa ufanisi na tija, vinasimamiwa na kuhifadhiwa kwa umakini. Kasimamie Sheria, Kanuni na Miongozo ya Utumishi wa Umma.

Kwa Mkurugenzi wa Mipango, Wahasibu, Wanunuzi na Wagavi, Wakaguzi wa Hesabu, Wanahabari, Watu wa teknolojia. Kwa Wahudumu wetu, Watu wa Masjala, Maafisa Usafirishaji, Waandishi Waendesha Ofisi, Wakutubi na yeyote aliye katika utumishi kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali; ni rai yangu mkawajibike katika nafasi zenu na tuone matokeo bora ya kila mmoja wenu.

Wenzetu mlioko mikoani;
Ninyi ni sehemu ya Ofisi hii, msije kufikiri mko mbali au hamuonekani. Mkaenende inavyowapasa mkizingatia Kanuni na Miongozo ya Utumishi wa Umma; mkapatikane Ofisini wakati wote wa kazi na kuhudumia wananchi kwa bidii, ubora na staha; mkazingatie Miongozo ya Mavazi ya Watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali; na mkahakikishe na kuzingatia matumizi bora na yenye tija ya rasilimali za umma, hususani fedha na mali mbalimbali. Tunawaoneni wakati wote.

Ndugu Watumishi wenzangu wa OMMS,
Katika dunia ya sasa, inayokwenda sambamba na kasi ya mabadiliko ya kidijitali, matumizi sahihi ya mitandao ya kijamii si suala la hiari, bali ni nyenzo muhimu ya

maisha ya mwanadamu katika shughuli binafsi, kikazi na kibiashara. Kwa sababu hii, niwasihi kutumia mitandao ya kijamii ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa kuitembelea na kuifuatilia.

Kupitia ninyi, wadau muhimu katika mnyororo wa sheria na wananchi kwa ujumla watapata maarifa na uelewa kuhusu kazi zinazotekelezwa na Ofisi yetu.

Ndugu Watumishi wenzangu wa OMMS,
Ili kuyafikia malengo na shabaha ya Dira 2050, ni lazima sisi tukiwa washauri wa kisheria tukimbie mbele zaidi. Wakati wenzetu wengine wanakuja, wakute tayari tumezifungamanisha sheria zetu na malengo ya Dira 2050 kwa kuzifanya rafiki na wezeshi kwa sekta na malengo mbalimbali. Ili kulifikia lengo hilo, ni lazima kila mmoja wetu katika nafasi yake awajibike ipasavyo. Kwa sasa nyenzo zote tunazo, tunadaiwa matokeo.

Ndugu Watumishi wenzangu wa OMMS,
Naomba sasa nihitimishe hotuba yangu kwa kuwarai tena, twendeni tukakitumie kikao hiki vizuri kwa lengo moja tu la kuiwezesha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kwa wakati. Wakati wote tukiongozwa na kaulimbiu yetu “Weledi na Ubora”.

Tunayo Dira moja inayotekelezwa kwa mikono mingi. Twendeni tukajadiliane kwa ajili ya kuijenga zaidi Ofisi na nchi yetu kwa ujumla. Tukazungumze kama familia moja imara, ili baada ya hapa tukazidi kutekeleza majukumu yetu kama Timu moja.

Tuna mambo mengi na makubwa mbele yetu. Yakiwezekana, ni kwa sababu sisi watumishi wote katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali tunafanya kazi kwa ubora na kwa umoja.

Baada ya kusema haya, sasa naomba nikukaribishe Mgeni rasmi wetu Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria kwa ajili ya kutufungulia Mkutano wa Watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ……. !

Asanteni kwa kunisikiliza.